## TAARIFA KWA UMMA

## TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

1. Social Action Trust Fund (SATF) ni taasisi iliyoanzishwa mwaka 1998, kwa lengo la kusaidia juhudi za Serikali katika kutoa huduma kwa Watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kupunguza athari zitokanazo na ugonjwa wa UKIMWI. Kwa sasa SATF inafanya kazi katika mikoa 17 na Halmashauri 37 za Tanzania. Huduma zinazotolewa ni pamoja Elimu, Afya, Ulinzi wa Mtoto pamoja na afua za kuimarisha uchumi katika ngazi ya kaya.
2. SATF kwa kushirikiana na Chuo Cha Maendeleo Cha Msaginya - imeandaa mafunzo ya muda wa miezi mitatu (3) yatakayofanyika katika Chuo Cha Maendeleo Cha Msaginya kilichopo Wilaya ya Nsimbo,Mkoani Katavi . Fani zitakazotolewa katika mafunzo hayo ni pamoja na;- ***Umeme wa Majumbani***, ***Ushonaji na Kutarizi***, ***Uashi/Ujenzi***, ***Ufundi Magari***,***Kilimo na Uselemala***.

3. SATF inapenda kuwatangazia Vijana wa kitanzania wenye umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25 katika Wilaya zifuatazo; Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mkoani Tabora kutuma maombi ya kujiunga na mafunzo haya.

   SATF itagharamia gharama zote za mafunzo haya ikiwa ni pamoja na ada, malazi pamoja na chakula kwa muda wote wa mafunzo.
4. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi inayopatikana katika ofisi za shirika la TDFT - Tabora ama katika ofisi ya Afisa Maendeleo wa Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ama katika tovuti www.satf.or.tz. Fomu iliyojazwa irudishwe katika ofisi mojawapo kati ya Ofisi ya Afisa Maendelo wilaya unayotoka au ofisi za TDFT- zilizopo Manispaa ya Tabora , kabla ya tarehe 3 Septemba,2026

5. Fomu za maombi ziambatane na nyaraka zifuatazo;
    i. Kitambulisho cha uraia au kadi ya mpiga kura,
    ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa au kiapo cha ushahidi wa kuzaliwa,
    iii. Barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji anakoishi mwombaji; na
    iv. Picha mbili za paspoti *(ziandikwe majina matatu ya mwombaji kwa nyuma)*
6. Sifa za kujiunga na mafunzo haya ni:
    i. Awe Mtanzania mwenye umri wa miaka isiyopungua 18 na isiyozidi 25
    ii. Awe kijana nje ya shule aliyemaliza Elimu ya msingi au sekondari
    iii. Awe na nia ya dhati ya kujifunza ujuzi aliouchagua.
    iv. Awe tayari kujiunga kati ya kozi mojawapo tajwa.
    v. Vijana wenye ulemavu na wanaotoka kwenye kaya zilizo chini ya mpango wa TASAF na SATF wanasisitizwa kuomba fursa hii na watapewa kipaumbele katika mafunzo haya.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi SATF**
**20 Agosti, 2026**

***NB:***

- ***Watakaokidhi vigezo na masharti tu ndio watakaochaguliwa***.
- ***Maelekezo zaidi na taratibu zote za kujiunga yanapatikana pia kwenye ofisi za TDFT-Manispaa ya Tabora - Bi. Magdalena Kwaang 0615 212 708 au Bi Joselina Mutoka 0768 026 544.***